# HALMASHAURI YA TAIFA YA MAZAO-1963-1971

MAZAO

# HALMASHAURI YA TAIFA YA MAZAO-1963-1971

## *HISTORIA FUPI YA KUUNDWA KWA HALMASHAURI YA TAIFA YA MAZAO:*

Kabla ya Tanzania kupata uhuru, serikali ya kikoloni ilijiingiza sana katika mazao ya biashara na nchi za nje na haikujali sana juu ya mazao yaliyotumika humu nchini hasa yale ya chakula ambayo wananchi hutumia. Siasa yao ya kikoloni wakati huo ilikuwa kukuza mazao ambayo yangeuzwa na kukuza uchumi wa nchi zao. Siasa hiyo kwa kweli iliweza kuleta madhara kwa mazao ambayo yangetumika au kuliwa humu nchini, kwa hiyo upanuzi wa kilimo cha mazao machache kuliifanya Tanganyika kutegemea mazao kama katani na kahawa kuwa mazao makuu ya biashara na nchi za nje.

Katika sehemu za mashambani, wananchi waliendelea kulima mahindi, mpunga na vyakula vingine ambavyo ni vya muhimu. Mazao hayo yalitumiwa pia kuinua uchumi wao, na kila kilichobaki waliuza katika masoko yao ya mijini au vijijini kupata fedha. Hata hivyo, wananchi walibakiwa na vyakula vya kutosha kwa mahitaji yao ya nyumbani.

Upungufu wa uchumi wa fedha katika Tanganyika na sehemu zingine za ulimwengu, pia utengenezaji wa vitu mbalimbali, uliondoa zile njia za zamani za uchumi. Watu walivuna mazao yao na kuuza kwa wafanya biashara ambao walilipa fedha mara moja, na kutumia fedha hizo kwa kununulia nguo na vitu vingine vya lazima katika maisha yao. Kwa sababu ya kishawishi cha kupata fedha mara moja, wakulima wengi waliweza kuuza chakula chao hata kile ambacho waliweka akiba ya baadaye, kwa bei ya chini sana. Kwa bahati mbaya wakati hali ya hewa ilipokuwa mbaya, mazao mengi hayakustawi na watu wakaingiliwa na njaa. Haikuwezekana kupata msaada wa chakula kwani chakula chote kilichouzwa kwa wafanya biashara walikwisha kuuza katika nchi za nje na kujipatia faida kubwa. Hata kama kulikuwa na chakula kilichobaki, kiliuzwa kwa mkulima kwa bei iliyozidi mara nne(4) ya ile bei ambayo mkulima aliuza kwa mfanya biashara huyo. Kuingiliwa na njaa kulilazimisha nchi hii kuagiza mahindi kwa wingi toka nchi za nje kwa bei kubwa. Licha ya hiyo, serikali ililazimika kujiingiza katika ugawaji wa chakula katika sehemu zilizoingiliwa na njaa.

Wakati ununuzi wa mazao ya mahindi na mpunga ulikuwa mikononi mwa watu binafsi, bei ya mazao hayo ilikuwa daima inatofautiana. Mkulima hakuweza kulindwa kutokana na tofauti hii ya bei, hakuweza kuwa na sauti katika ununuzi na uuzaji wa mazao hayo, hivyo mkulima Mtanganyika ndiye aliyeumia zaidi kwani hakuwa na uwezo wa kujipigania katika soko la dunia na wala kufanya mashindano na mataifa ambayo yalikuwa yakifanya biashara kwa muda mrefu uliopita. Kutokana na matatizo hayo, ilikuwa ni lazima kwa serikali huru ya wananchi kutafuta njia za kumaliza dhuluma hii. Ilionekana kuwa mkulima asiachwe kuwa kama mkosaji kufuatana na siasa tuliyoachiwa hapa Tanganyika wakati ule.

2. *MADHUMUNI:*

Licha ya tofauti za bei na njaa ambayo ilitokea mara kwa mara sababu ya wafanya biashara wachoyo, kulikuwepo pia sababu nyingi ambazo ziliifanya serikali ijiingize katika masoko ya mazao yetu.

Kwanza, serikali ya wananchi ilitambua mapema kabisa kuwa hali ya maisha ya wananchi na mabadiliko ya uchumi nchini; kufutwa kwa utaratibu wa uuzaji na ununuaji wa mazao nchini, ukuzwaji wa soko la ndani na uangalizi wa jumla wa maisha ya watu unaweza kutimizwa kwa kuanzisha utaratibu wa masoko kupitia bodi maalum za biashara.

Pili, serikali iliona kuwa ilikuwa na wajibu wa kulinda haki za wakulima na walaji kutokana na upungufu wowote ambao ungetokea katika soko la dunia na hivyo kukuza hali yetu ya uchumi.

Tatu kulikuwa na haja kwa serikali kutimiza wajibu wake wa kulisha taifa wakati itokeapo njaa, na kuhakikisha kuwa ugawaji wake umefanyika vema,

Nne, kama kulitokea mabadiliko yoyote ya hewa juu ya mapato na ukosaji wa vyakula ilikuwa ni lazima kuwa na shirika lenye uwezo kamili wa kuweka akiba, na kama akiba haitoshi basi ni juu ya shirika hilo kuagiza chakula toka nchi za nje.

Tano, kulikuwa na haja ya kumwondoa mtu wa kati ambaye aliwakandamiza wakulima kwa kutoa bei ndogo na kusingizia juu ya mabadiliko ya bei katika soko la dunia.

Sita, ujengaji na uimarishaji wa maghala kwa utunzaji bora wa mazao ilionekana kuwa ni jambo la lazima.

Mambo hayo yote ya juu iliifanya serikali ijiingize katika mipango na utaratibu wa masoko kwa kuanzisha mashirika maalum, mojawapo likiwa hili la Halmashauri ya Taifa ya Mazao (National Agricultural Products Board).

### 3 *SHERIA:*

Kutokana na msingi huu, sheria ya kuundwa Halmashauri ya Taifa ya Mazao ilitungwa mwaka 1962. Sheria hii iliimarishwa zaidi na usemi wa Waziri waKilimo Mheshimiwa D. N. M. Bryceson, ambao ulisema:–

"Ni maoni ya serikali hii, Bwana Spika, kuwa ili tupate utaratibu bora kwa mkulima kuuza mazao yake, uangalizi mkubwa unahitajika. Tunahitaji utengemano zaidi wa bei ya mazao yetu. Hii hatuwezi kufanya kwa siasa tu katika biashara yenyewe, bali ni nia yenyewe ambayo Serikali imeleta katika bunge hili, kuweza kuhimiza maendeleo ya vyama vya ushirika na kukuza vile ambavyo vipo sasa. Nimetaja pia sababu nyingine kuhusu sheria hii, nayo ni kwamba tunaweza kupata nyongeza bora ya bei ya mazao yetu ambayo itatuwezesha kufanya mipango ya baadaye ya maendeleo yetu".

Maelezo hayo yanamaanisha kuwa haitoshi tu kuongeza mazao yanayolimwa, lakini pia mipango ya kufaa ya uuzaji wake lazima ifanywe, ili hata kama nchi yetu itapambana na tatizo la kupungua bei katika soko la ulimwengu tuweze kulipa bei nzuri kwa mazao yale, kwani wananchi walikwisha fanya wajibu wao katika kukuza uchumi wa nchi.

Sheria ya mazao ya Kilimo ya mwaka 1962 (Marketing & Control Act, 1962) iliweka msingi wa jinsi bodi mbalimbali

zinavyoweza kuanzishwa kwa Mwongozo utakaotolewa na Waziri wa Kilimo. Ilikuwa sababu ya mwongozo huu, ndipo Halmashauri ya Taifa ya Mazao ikaundwa mwaka 1963. Ili kutimiza lengo hilo, Halmashauri hii ikakabidhiwa madaraka yafuatayo: —

(a) Uwezo wa kushughulika na masoko na kupanga bei za mazao ambayo bodi huangalia na kutoa mwongozo wa kisheria.

(b) Uwezo wa kukopa fedha za kuanzisha na kuweka akiba ya fidia ya tofauti ya bei ya mazao, kudumisha bei ya mazao na kulinda soko la mazao ya wakulima.

(c) Uwezo wa kutawala uingizaji na uuzaji wa mazao yanayoangaliwa na bodi.

(d) Uwezo wa kutunza na kupanga gredi kwa mazao yanayoangaliwa na bodi.

(c) Uwezo wa kutawala uingizaji na uuzaji wa mazao yaliyo chini yake.

(f) Uwezo wa kuanzisha mfuko maalumu wa kusaidia urekebishaji wa bei za mazao yanayouzwa katika maso-ya nchi za nje.

(g) Uwezo wa kutoa liseni (licence) kwa wasagaji na wagawaji, pia kuingiza nchini au kutoa nje liseni kwa mazao yaliyo chini yake.

(h) Uwezo wa kukagua majumba au magari ambayo hudhaniwa kuwa yameweka vyakula vinavyoangaliwa na Halmashauri ya Taifa ya Mazao.

Sasa ebu tuone jinsi Halmashauri ya Taifa ya Mazao ilivyofanikiwa katika lengo hilo kwa muda wa miaka tisa (9) iliyopita tangu iundwe.

Katika kufikia lengo hilo, Halmashauri ya Taifa ya Mazao ilifuata misingi na ukweli kuwa maendeleo ya Kilimo huhusika pia na maendeleo ya uchumi kutokana na nchi zingine, kupitia vifaa na utumishi unaotakiwa mahala pengine kiuchumi, na uuzaji, kupitia uwezo wa watu wanaonunua vitu vijijini. Jambo jingine lililochunguzwa na Halmashauri ya Taifa ya Mazao ni kwamba, ili kumlipa mkulima haki ya jasho lake, na wakati huo huo kutunza usawa wa bei kati ya mkulima na mlaji, ilikuwa lazima izingatie siasa ya kupunguza gharama.

Zao la kwanza lililomilikiwa na Halmashauri yaTaifa ya Mazao ni Mahindi. Miaka iliyofuata serikali ikaamua kuingiza mazao mengine katika Halmashauri hii na kuongeza madaraka ya Halmashauri hii. Leo licha ya mahindi, mazao mengine kumi na moja zaidi yanamilikiwa na Halmashauri ya Taifa ya Mazao, nayo ni:— Mpunga, Karanga, Ufuta, Nyonyo, Alizeti, Korosho, Ngano, Iliki, Mhogo, Mtama na Uwele. Hivyo, licha ya Halmashauri hii kushughulikia mazao ya chakula, pia imepewa madaraka ya kuuza mazao mengine ya kibiashara ndani na nje ya nchi yetu.

# SURA YA PILI

## *MIPANGO YA UUZAJI WA MAZAO*

*(1) Uhusiano kati ya Halmashauri ya Taifa ya Mazao na vyama vya Ushirika.*

Hali ya Halmashauri ya Taifa ya Mazao katika muundo mzima wa njia za ugawaji Mazao yaweza kuelezeka kifupi vifuatavyo:— Kwa kawaida, Halmashauri ya Taifa ya Mazao au nyingine ya aina hiyo ni Halmashauri ambazo kazi zake ni kutoa huduma ya uuzaji bora wa Mazao ya Wakulima. Kabla ya kuanzishwa kwa Halmashauri hizi za uuzaji, wakulima hawakuwa na sehemu ya utaratibu huu wa uuzaji, wala hawakuweza kuelewa na kufuatisha uelekeo wa Mazao yao, au kujua bei Mazao hayo yalivyouzwa hatimaye. Iliwalazimu kuthamini uuzaji wa Mazao yao kwa wafanya biashara binafsi. Upotovu huu wa utaratibu maalumu wa uuzaji mazao uliwadhuru sana wakulima pamoja na wanunuzi na walaji ingawaje wale wachuuzi au wafanya biashara wachoyo walifaidika mpaka ikahisiwa kuwa sharti hawa wachuuzi waondoshwe kwa kuunda Mashirika ya uuzaji Mazao ya umma na kuyaunganisha Mashirika hayo chini ya utaratibu mmoja. Mashirika haya mapya yaliyoundwa ndiyo Vyama vya Ushirika na Matawi yake, Halmshauri za uuzaji Mazao, Shriika la taifa linaloshughulika na usagaji wa Mazao (National Milling Corporation) na Shirika la Ugawaji la Taifa (National Distributors Ltd.) lilipoundwa njia zote za uuzaji hata za reja reja ziliingia mikononi mwa Mashirika ya umma. Wizara ya Kilimo na vyama vya Ushirika ilitenda kama "Mzazi" ikiunganisha au kupatanisha pamoja na kuelekeza pamoja shughuli za Mashirika yote yaliyotajwa hapo juu.

Mpango wa awali ulikuwa kuanzisha vituo vidogo vidogo vingi vya ununuaji Mazao ambayo vilikuwa karibu ya kutosha na makazi ya Wakulima wenyewe katika sehemu kuu za uzalishaji Mazao. Hii inamaanisha ya kuwa Wakulima walipatiwa njia ya kuweza kuuza Mazao yao yote na kwa bei ya kuwafaa.Vituo hivyo vya ununuaji Mazao toka kwa Wakulima vimetapakaa nchini pote

na vinaendeshwa na Vyama vya Ushirika vya Wakulima au na Matawi ya Shirika hili. Shirika hili linayo Matawi mengi yatumikayo kama vituo vya ununuzi Mazao, na katika sehemu zisizokuwa na Matawi ya Shirika hili Vyama vya Ushirika vikisaidiwa na Matawi yake hutekeleza shughuil zote za ununuzi mpaka hatua ya uchukuzi wa Mazao hadi kwenye mabohari makuu ya Shirika hili. Ili kurahisisha ulinganifu au upatanishaji wa shughuli, vyama hivyo hivyo vya Ushirika pamoja na Matawi yake hutumiwa kama wakili wakubwa wa Shirika hili. Mzunguko huu wa Mazao kupitia matawi ya vyama vya Ushirika, hadi Shirika la Mazao la Taifa ndiyo tu njia iliyopo ambayo inatambulika kiserikali. Hapo awali wakulima pekee waliojiweza waliruhusiwa kuvipitiliza vyama vya Ushirika na kuliuzia Shirika hili Mazao yao moja kwa moja, lakini mpango huu sasa umezuiliwa.

Tangu hapo imekuwa ni wajibu wa Halmashauri hii kutafuta Masoko kwa ajili ya Mazao ya Kilimo. Wajibu huu hutekelezwa kwa njia kadha wa kadha kutegemea kama zao lenyewe au Mazao yenyewe ni kwa ajili ya ulaji wa hapa hapa nchini au ni kwa ajili ya uuzaji kwa nchi za nje. Mazao kwa ajili ya matumizi ya hapa hapa nchini, kama vile mchele, Mahindi na Ngano, huuzwa kwa bei maalum, zilizorekebishwa na serikali. Huuzwa kwa Shirika lishughulikalo na Vinu vya usagaji na usindikaji wa Mazao ya chakula (National Milling Corporation), na Mashirika mengine kama hayo, ya Vyama vya Ushirika. Baada ya kusaga Mazao hayo, Shirika hilo la usindikaji na usagaji (NMC) huuza unga huo kwa wafanya biashara wa jumla wenye leseni maalum ya ugawaji. Mazao kama Korosho, Ufuta na Iliki huuzwa nchi za nje na Shirika la Mazao. Mara nyingine sehemu ya Mazao hayo ya kuuzwa nchi za nje huweza kuuzwa hapa hapa nchini kwa Viwanda fulani fulani kama vile itokeavyo kwa zao la Korosho.

Jambo la kuangaliwa kutokana na maelezo haya ni ule uhusiano kati ya Vyama vidogo vya Ushirika, vyama vikuu vya Ushirika, Halmashauri za uuzaji Mazao (Marketing Boards) watayarishaji na wasagaji (Millers) pamoja na wagawaji Mazao, na jinsi vitu hivi vinavyounganishwa na kuhusiana. Kwa hiyo ni wazi kwamba utaratibu maalum wa uuzaji Mazao upo kuanzia ngazi ya mkulima hadi kwa mnunuzi mlaji wa mwisho. Wajibu na shughuli za Wizara ya Kilimo katika jambo hili ni ya maana sana, kwani

Wizara huunganisha na kupatanisha shughuli hizo, na hushauri na kuongoza Mashirika na kuyapa misaada katika mambo mengine. Hata hivyo, Halmashauri imehisi umuhimu wa kutafakari na kuchungua tena uhusiano wa utaratibu kati ya Vyama vidogo na vikubwa vya ushirika na Halmashauri yenyewe. Wakulima wakae wakijua kwamba Serikali imekwisha ona haja ya tafakari au uchunguzi huo na hatua za mwanzo kufikia lengo hilo zimekwisha chukuliwa.

Uanzishaji wa utaratibu huu wa mkondo mmoja wa ununuzi wa Mazao toka kwa mkulima hadi kwa mnunuzi mlaji wa mwisho au hadi kwenye Masoko ya nchi za nje, ulihitaji mpango wa ununuzi na ugawaji (yaani mpango wa Masoko) ulio mgumu na wa kutatanisha sana. Ulihitaji Soko lenye Mashirika mbali mbali yanayo husiana katika ngazi na viwango mbali mbali, kila Shirika likiwa na shughuli maalum ya kutekeleza.

Kielelezo kifuatacho kitatusaidia kufafanua kazi za Mashirika hayo mbali mbali yanayohusika, na uhusiano uliopo baina ya Mashirika hayo, yenyewe kwa yenyewe: —

WAKULIMA
|
VYAMA VIDOGO VYA USHIRIKA
|
VYAMA VIKUU VYA USHIRIKA
|
HALMASHAURI YA MAZAO
|
UUZAJI
/ NDANI — KWA JUMLA — WASAGAJI \
/ / /
VIWANDA — UGAWAJI
/ /
UGAWAJI, VYAMA VYA USHIRIKA n. k.
— — — — — — — — — — — — — — —
|
V
WALAJI

*(2) UBORA WA MAZAO.*

Kwa kuwa Mazao ya Kilimo ndiyo nguzo ya sehemu kubwa ya bidhaa ziuzwazo na nchi yetu katika Masoko ya nje, basi ubora

wa Mazao, licha bei yake, hauna budi kuwa kiini cha maana sana katika shughuli zetu za uuzaji wa Mazao nchi za nje. Ikiwa tutaachia ubora wa mazao yetu kushuka, thamani ya mazao hayo na ufanisi wetu katika uuzaji wa mazao nchi za nje vitashuka na hii itasababisha ukosefu wa fedha za kigeni ambazo tunazihitaji sana kununulia bidhaa za Ng'ambo kama Mashine na vifaa, dawa na vyakula. Ni vema pia kuelewa umuhimu wa kuhifadhi na kudumisha ubora wa Mazao ya Kilimo ya kuuzwa nchi za nje hasa tufikiapo kuwa katika biashara ya mashindano iliyopo katika soko la Dunia, ni Mazao yale tu yaliyo bora zaidi ya mengine ndiyo yanayoweza kuuzwa katika bei ya kulinganishwa. Kanuni hii imekuwepo hadi leo na itazidi kuwepo siku zijazo. Ufanisi wetu katika kuuza nje Mazao bora itategemea sana uwezo wa wakulima wetu (wote, wala sio wachache wao) kukifikia kiwango cha ubora kilichowekwa kwa kila mojawapo ya Mazao yetu ya kuuzwa nchi za nje. Hii ndiyo sababu ya juhudi zetu nyingi za kumwelimisha kila Mkulima juu ya haja na umuhimu wa kuzizingatia hatua za udumishaji na uhifadhi wa ubora wa Mazao ambazo zimekuwa zikielezwa kwao na mabwana–shamba pamoja na ma–afisa wa Ushirika (Cooperative Officers.)

Kwa ajili ya wasomaji wetu na hasa jumuia yote ya wakulima, tutaandika hapa chini kwa kifupi, kanuni za Shirika zitumikazo kupimia daraja mbali mbali za ubora wa mazao machache yauzwayo hapa hapa nchini, na mengine yapelekwayo Masoko ya nje: —

(*1*) *Mahindi:*

(a) Daraja la kwanza (grade 1) — Mahindi meupe:— Unyevunyevu wake (Moisture Content) usizidi sehemu 13 kwa mia. Mahindi yenye unyevunyevu ufikiao 15% yaweza kupokelewa kwa utashi wa Shirika, lakini, kwa kila ½% inayozidi 13% nusu kilo itakatwa katika uzito wa kila gunia wakati wa kupimwa, Michanganyiko iliyopo katika Mahindi hayo isizidi sehemu moja ya mia 1%, michanganyiko ya rangi nyingine mbali ya nyeupe isizidi sehemu 10 kwa mia, 10%.

(b Daraja la pili (Mahindi njano — Yellow Maize, kanuni

za upimaji ni kama zile za daraja la kwanza na mchanganyiko sehemu 10 kwa mia — 10%.

(c) Daraja la tatu (Mahindi mchanganyiko) kanuni za upimaji pia ni kama zile za daraja la kwanza, na michanganyiko wa rangi nyingine mbali na hizo kuu usizidi 10%.

(d) Daraja la nne (Mahindi hafifu) Mahindi ya rangi nyingine zozote na michanganyiko inayozidi 15% lakini ambayo bado yafaa kuliwa na binadamu.

(2) *Mchele*: —

(a) Daraja la juu (Standard grade – AFAA, FAYA) wenye punje ndefu na rangi moja.

(b) Daraja la chini (Bora kupata na maji maji) Hizi ni aina za mchele wenye punje fupi fupi. Mchele mwingine ambao hauambatani na kanuni hizi za upimaji lakini ufaao kuliwa, pia unahesabiwa katika hili. Mchanganyiko wa aina nyingine usizidi 10%, na kiasi cha punje zenye kasoro kisizidi 10%. Vipimo pishi visizidi ratili 40 kila kipimo, na unyevunyevu usizidi 13%. Jumla ya mchele mbovu uliopo usizidi 15% na kati ya hii, kiasi cha mchele uliopekechwa au kuliwa na wadudu isizidi 10%.

(i) Michanganyiko ya taka za aina nyingine isizidi 2%.

(ii) Mchele mbovu usizidi 3%.

(iii) Kipimo pishi kisizidi uzito wa ratili 45.

(iv) Unyevunyevu usizidi 13%.

(v) Punje zilizovunjika au kusagika wakati wa kutwanga zisizidi kiasi cha 10% ya uzito wa mchele.

(vi) Mchele wa aina nyingine ya punje fupi, mbali na huo unaoambatana na aina hizi mbili zilizotajwa pia watambulika.

(3) *Mazao ya aina ya Mafuta. (Oilseeds)*

Mambo ya lazima: — Zao lilingane na wastani wa ubora wa Zao lenyewe kwa jumla (Fair Average Quality) liwe kavu na safi lisilokuwa na takataka nyingi. Mazao ya aina ya mbegu za mafuta mbali ya nyonyo yasiwe na michanganyiko ya nyonyo au mbegu nyingine za mafuta zitumikazo kutengenezea dawa. Mbegu za aina ya mafuta lazima zisiwe na koyu, chachu au wadudu.

(a) Karanga:— Unyevunyevu wake usizidi 9%, na wingi wa taka na michanganyiko usizidi 1%.

(i) Karanga za kulika (Veluets & Dodomas) kiasi cha michanganyiko ya aina nyingine kisizidi 5%. Kiasi cha punje zilizo sinyaa au kukunjama kisizidi 12%.

(ii) Karanga mchanganyiko aina ya Mtwara na Azania, kiasi cha punje za kusinyaa kisizidi 12% katika mchanganyiko wa aina nyingine usiozidi 25%.

(b) Nyonyo: — Kiasi cha takataka kisizidi ½%.

(c) Ufuta:— Kiasi cha takataka kisizidi 1½%

Mbegu za Ufuta hupangwa makundi matatu kufuatana na kanuni hizi: —

(i) Tanzania White (nyeupe) — rangi nyingine zisizidi kiasi cha 10%.

(ii) Tanzania Black (nyeusi) — rangi nyingine zisizidi kiasi cha 10%.

(iii) Tanzania Mixed (mchanganyiko) — Ufuta wowote ambao unaambatana na kanuni za kawaida za kupima ufuta lakini zisizoingia hasa kwenye aina hizo mbili —nyeupe na nyeusi.

(d) *Alizeti:-*

Hizi ni kanuni za kawaida zinazo tumika kupima aina zote za alizeti kiasi cha takataka kisizidi 1%. Kiasi cha jumla ya punje mbovu (Kuacha zilizopauka rangi)

kisizidi $1\frac{1}{2}\%$. Kiasi cha jumla ya punje zilizopauka rangi kisizidi 8%.

Alizeti ipo aina tano kufuatana na kanuni hizi.

(i) Alizeti Nyeusi — rangi nyingine zisizidi kiasi cha 5%.

(ii) Jupiter — aina nyingine zisizidi kiasi cha 5%.

(iii) Alizeti Nyeupe — rangi nyingine zisizidi kiasi cha 5%.

Zenye zaidi ya 8% ya punje zilizopauka au kugeuka rangi yeweza kupangwa katika daraja la Alizeti Nyeupe (White Sunflowerseed).

*DARAJA LA II*

(iv) *"Comet"* — sio zaidi ya 5% ya aina nyingine inaruhusiwa.

(v) Iringa Mchanganyiko — zisiwepo punje nyeusi zaidi ya kiasi cha 35%.

(vi) Tanzania Mchanganyiko — Alizeti yoyote inayoambatana na kanuni za kawaida za upangaji wa alizeti lakini zisizoingia kwenye makundi yale matano yaliyokwisha tajwa.

(4) *Korosho*:

(a) Daraja la juu linalotambulika na Shirika. Punje zote za Korosho hazina budi kuwa safi, zisizo na takataka na ambazo zimekaushwa juani kwa muda usiopungua siku tatu mfululizo. Zisiwemo mbegu changa, zilizopauka au kugeuka rangi, ama zilizopekechwa au kutiwa kovu. Mpaka sasa hamna njia inayojulikana ya kuweza kupanga daraja za Korosho katka maganda yake. Ifuatayo ndiyo njia (Ingawaje si sahihi ila ya makisio tu) itakayoweza kuvisaidia Vyama vya Ushirika katika kupanga daraja za Korosho:—

*Njia ya kusikia*:—

Punje za Korosho zilizo kaushwa juani siku tatu mfululizo hutoa sauti ya kudata zitingishwapo.

*Takataka*:—

Masalia ya nyama ya bibo kwenye punje ya Korosho huhesabika kama uchafu wa Zao. Punje mbovu zisizidi kiasi cha 12% na hata hizo pia ziwe kavu na safi. Unyevunyevu wa Zao usizidi 12%.

(b) *Daraja la chini*: —

Korosho nyingine zozote kuacha ambazo zimeoza na/au teketeke. Pia kiasi cha Korosho mbovu zilizochanganyika ndani zaidi ya 13%.

Ikiwa na nia ya kuzitekeleza kanuni ya viwango vya ubora wa Mazao zilizokwisha tajwa, Halmashauri ikiwakilishwa na kamati yake ya ukaguzi, imekuwa inavitumia vikundi vya wakaguzi wa Mazao (Produce inspectors), na vikundi vya kushughulika na kuua wadudu wanaoshambulia Mazao (Fumigation and Pest — Control Units), kutumia dawa za kuua wadudu. Hao wakaguzi wa Mazao wakishirikiana na Mabwana — Shamba wa Idara ya Kilimo, pia wamekuwa wakitoa mawaidha na mafunzo kwa vyama mbali mbali vya Ushirika, vidogo na vikubwa, nchini pote. Zaidi ni kutokana na juhudi zao kwamba Halmashauri imefaulu sana kupata ushirikiano wa Wakulima na vyama vya Ushirika, katika kudumisha na kuzidisha ubora wa Mazao yao. Katika kuiendesha mipango hii ya kuongeza ubora wa Mazao kwenye wakati huo unaozungumziwa, Halmashauri hii ilitumia jumla ya Shilingi 2,195,394/60 ambazo ziligawanywa vifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1963/64 | Shs. 123,300/- |
| 1964/65 | Shs. 399,830/- |
| 1965/66 | Shs. 122,273/- |
| 1966/67 | Shs. 379,827/- |
| 1967/68 | Shs. 494,360/- |
| 1968/69 | Shs. 450,182/25 |
| 1969/70 | Shs. 216,622/35 |
| Jumla: | Shs. 2,195,394/60 |

Zaidi ya shughuli hizi za kudumisha ubora wa Mazao, Halmashauri imevipa vyama vya Ushirika Mashine za kupimia unyevunyevu wa Mazao (moisture meters) bure bila malipo yoyote, ili zisaidie katika kazi ya upimaji wa Mazao. Halmashauri pia imeweka mashine za kukaushia Korosho Dar es Salaam na Mtwara na zaidi ya hayo imechanga kiasi kikubwa cha fedha za kuhudumia vituo vya uchunguzi vinavyoshughulika na utaalamu wa njia za kuendeleza ubora wa Mazao.

Katika kuongeza kiwango cha ubora wa Mazao, Halmashauri hupimia ubora wa kiasi fulani kwa gharama isiyozidi sana, na pia imefikiria mahitaji ya mnunuzi—mlaji ambayo hutegemea uwezo wake wa kulipia gharama za ubora wa zao lenyewe zilizopo katika kima cha kuweza kutosheleza mahitaji yake. Kwa upande wa mkulima, lingalikuwa si jambo la busara kuweka kiwango cha juu sana ambacho kingalifikiwa tu na wakulima wachache watumiao njia za kisasa na za hali ya juu sana za ukulima. Pia isingalifaa mnunuzi kama kiwango cha ubora kilichowekwa kitapandishwa bei ya zao ama bidhaa yenyewe kiasi ambacho ni juu ya kima cha kadiri kiwafaacho wanunuzi walio wengi. Yafaa ieleweke kwamba njia za kupimia ubora zilizoelezwa hapo juu hutumiwa zaidi na Halmashauri ya Taifa ya Mazao. Wakulima hawawezi kutegemewa kuzitumia njia hizo za upangaji wa daraja za Mazao, ambazo ni za kitaalamu sana. Badala yake sheria hizo hutumiwa na wafanya kazi wa Halmashauri wanaoshughulika na kupanga daraja za mazao ambayo huuzwa humu nchini ama kwenye masoko ya nje. Hata hivyo, kanuni za upangaji daraja za Mazao ambazo hutayarishwa na Halmashauri ya mazao kwa vyama vya Ushirika kila mwanzo wa msimu nazo huandikwa kwa njia rahisi ambayo yaweza kueleweka vema na kuweza kufuatwa na wakulima. Halmashauri pia imekuwa ikiwauzia wakulima kwa bei nafuu, mbegu maalum zilizochaguliwa ili kuwawezesha Wakulima kutoa mazao bora zaidi.

Kutokana na sheria thabiti za Halmashauri ya Taifa ya Mazao zinazorekebisha ubora wa mazao, mazao ya korosho na mbegu za mafuta kutoka Tanzania yamekuwa yakipata sifa kubwa ya ubora, katika soko la dunia, na bei za mazao ya Tanzania zina-

lingana vema na za Mazao ya nchi nyingine ambazo zimeendelea zaidi kiuchumi ingawaje kuna mashindano makali katika masoko ya dunia baina ya nchi mbali mbali. Baada ya kuzisoma sheria au hali za ubora wazitakazo wanunuzi wa nje wa Mazao yetu, bila shaka utaweza sasa kuzithamini sababu zinazo ilazimisha Halmashauri hii kupitisha hatua za kudumisha na kuongeza ubora wa Mazao. Kwa kifupi nia yetu katika kurekebisha ubora wa Mazao ni tuweze kutoa mazao kwa ajili ya wanunuzi wetu wa nchi za nje yenye thamani na kiwango cha ubora ambacho kinatambulikana katika masoko ya dunia. Ni kwa kutoa mazao bora zaidi, ndivyo tutakavyoiwezesha Tanzania kuongeza sehemu yake ya soko kwa ajili ya mazao yake. Hii tu ndiyo njia ya kumwezesha mkulima kuongeza kipato chake kutokana na mazao yake, na kuongeza kipato chetu cha fedha za kigeni ambazo zitatufaa katika kuinua hali ya maisha ya wakulima na wafanya kazi wa nchi yetu.

(3) *Urekebishaji wa bei*:

Urekebishaji wa bei za Mazao ya kilimo ni kazi ngumu sana hasa kwa Mazao ambayo bei zake hutegemea upandaji na ushukaji wa bei katika soko la dunia. Ushukaji bei huo unaweza kusababisha kuanguka vibaya kwa kipato cha fedha za kigeni kwa nchi, kama ilivyotokea hapo awali kutokana na kushuka bei za Korosho, Mchele na Iliki. Hali ya bei ya ndani ya nchi ya zao fulani, bei isiyobadilika yaweza kusababisha zao hilo lisiweze kushindana kwa ununuliwaji na mengine ya aina hiyo hiyo katika soko la dunia wakati wa mwaka wa mazao mengine. Tukichukua mfano wa Mchele, Halmashauri inashindwa kuuza ziada iliyopo ya mchele kwa nchi za nje kwa sababu, licha ya matatizo mengine, bei yetu ya mchele si ya kufaa kushindana na bei zilizopo katika soko la dunia kiasi cha kutosha. Bei ambayo Halmashauri ingependa kuipata kwa kuuza mazao nje ni bei ya mazao hayo (Mchele) yangalipo boharani pamoja na gharama za usafirishaji na utunzaji wa Mazao hayo; yaani bei ya mazao hayo yakiwa boharini yenyewe ni kubwa kuliko bei iliyopo ya ununuzi wa Mchele katika Masoko ya dunia. Hata hivyo tukitaka kuuza ziada iliyopo ya Mchele kwa Masoko ya nje, kwa bei ya chini kuliko hiyo

ambayo tungaliitaka, itatubidi kupata hasara ambayo itabidi kukabiliwa na Wakulima, ama wakulima pamoja na wanunuzi-walaji. Hivi itatubidi kutafuta kibali cha Kamati ya uchumi ya Baraza la Mawaziri (ECC) kuhusu mfuko wa kusawazishia bei za mauzo ya Mazao kwa Masoko ya nje (Export Equalisation Fund), kabla ya kuuza ziada hiyo kwa bei ya chini. Tangu tulipopata kibali hicho cha ECC tumeweza kuuza kiasi cha tani 8,000 kwa Kenya, Burundi, Zaire na Afrika ya Magharibi. Sababu hii mojawapo iliyoisababisha Halmashauri kutokuweza kuuza ziada yetu ya Mchele imeelezwa ili kuwaelewesha wasomaji wetu kwamba tuuzapo Zao lolote kwenye Soko la Dunia, wanunuzi wetu huamua kununua au kutonunua Zao letu kufuatana na uwezo wa bei pamoja na ubora wa Zao letu kushindana na Mazao mengine ya aina hiyo hiyo katika Soko la Dunia. Pia wanunuzi huweka maanani hali za wingi na utakiwaji (Supply and demand) wa Zao hilo kwa wakati huo, na mambo haya ndiyo hasa yanayorekebisha bei za Mazao yetu. Mnunuzi hajali wala hataki kujua kama bei zetu za ndani ya bohari pamoja na gharama za usafirishaji na utunzaji zitatoshelezwa na bei hiyo ama hapana. Kwa hali hiyo yoyote tumekwisha kujifunza kwamba thamani ya jitihada zetu, yaani hatua zetu zote zinazoendeleza kukubaliwa kwa Mazao yetu katika Masoko ya nje, ndizo ziamuazo kufanikiwa au kutofanikiwa kwa uuzaji wa bidhaa nchi za nje. Bei tunayoitaja ya mazao yetu ndiyo inayoamua uamuzi wa mnunuzi kununua Mazao yetu. Tukimtajia bei ya juu zaidi hatanunua; na huu ndiyo umaarufu wa bei ya bidhaa katika uuzaji wa Mazao yetu.

Kuhusu bei za mauzo na ununuzi wa Mazao ndani ya nchi yetu ambazo hulipwa kwa wakulima, tutaonyesha (Appendix A) orodha ya bei za kuuza na kununua zilizolipwa kwa wakulima kupitia kwenye vyama vyao vya Ushirika kwa muda wa miaka mitano iliyopita. Nia ya kuonyesha bei hizo ni kuwajulisha wanunuzi-walaji kwa ujumla, na hasa wakulima, bei zilizolipwa na Halmashauri kwa Vyama vikuu vya Ushirika ili vyama hivyo vizipitishe bei hizo hadi kwa wakulima wanachama, katika miaka hiyo mitano iliyopita.

Tunapenda kumalizia mazungumzo haya ya kuhusu bei kwa kuwajulisha waziwazi wakulima kwamba bei za ununuzi na mauzo

ya Mazao yatumikayo humu humu nchi hupewa kibali au huamuliwa na Kamati ya Uchumi ya Baraza la Mawaziri. Pia ni kweli kwamba misaada ya bei inayotayarishwa na Halmashauri hii kwanza hujadiliwa na kupasishwa na kamati maalum yenye wakili wa Wizara mbalimbali, ambayo hushughulika na kupatanisha na kuunganisha kazi za wizara mbalimbali, halafu ndiyo bei hizo hupelekwa kwa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Mawaziri (ECC) ili zipate kibali. Kwa hiyo ni wazi kwa wasomaji kwamba Halmashauri hii haiamui bei za Mazao yauzwayo hapa nchini ambayo yapo chini yake. Jambo jingine linalofaa kuelezwa wazi ni kuhusu bei zilipwazo kwa Wakulima. Kama ilivyokwisha kuelezwa hapo awali Halmashauri huwalipa wakulima bei zilizoelezwa bila kupungua wala kuzidi. Upunguzaji wowote wa bei za Mazao ufanywao na vyama vya Ushirika hauna budi kupata kibali cha awali toka kwa msajili wa vyama vya Ushirika (Registrar of Co-operative Societies).

Kuhusu bei za Mazao ya kuuzwa nchi za nje, Halmashauri haina uwezo wa kuamua bei za Mazao hayo kama vile ilivyo na nguvu ya kupendekeza bei za Mazao yauzwayo hapa nchini.

Nguvu tuliyo nayo na ambayo huwa tunatumia juu ya wanunuzi wa nje ni ile ya utoaji wa Mazao bora. Wanunuzi wengi wa nchi za nje hutoa uamuzi wao wa kununua Mazao kufuatana na ubora wa Mazao hayo wala sio kutokana na maelekezo ya mashirika yoyote ya mataifa. Huu ndiyo ukweli wenyewe tuliokwisha kuuona katika miaka kama tisa hivi iliyopita. Kwa hiyo kila mara tumekuwa tukitahadhari sana kwa kuweka bei za Mazao zivutiazo wanunuzi katika Masoko ya Dunia kama zile za washindani wetu. Kwa desturi huwa tunauza Mazao kwa niaba ya Wakulima, kwa bei ambazo huambatana na kiasi kizuri cha faida.

## *SURA YA TATU*

Kwa wakati huu wa kuadhimisha mwaka wa kumi wa Uhuru wa nchi yetu, inafaa Halmashauri kuangalia nyuma na kuchambua ufanisi wake katika wajibu iliyo nao wa kutunza na kuuza mazao ambayo yalikuwa mikononi mwake katika muda wa miaka tisa iliyopita. Tafakari hii ni ya juu juu tukiangalia shughuli mbali mbali za biashara, ambazo mara nyingine zilifanyika katika hali ya matatizo sana, katika miaka yote tangu 1963/64 hadi 1970/71. Tutajitahidi kutoa mambo ya kweli yaliyoonekana shughuli za kibiashara zilizofanywa na Halmashauri katika kipindi hicho kinachozungumziwa, tukiwazia lengo lililotajwa katika sura ya kwanza.

(1) Tangu mwaka 1964, kabla ya Azimio la Arusha, Halmashauri ilikuwa inashughulika kila upande katika ununuzi na uuzaji wa mazao, kuanzia hatua za ukusanyaji au ulimbikaji wa mazao (bulk-building), hadi za ugawaji au utawanyaji (bulk-bearing), tukihesabu mazao yale tu yaliyotajwa katika sura iliyopita. Kwa hiyo njia zote kubwa za kubadilishana mazao zilikuwa chini ya mikono ya Halmashauri ya Taifa ya Mazao.

Kwa upande wa ununuzi, Halmashauri ilishughulika na kiasi cha tani 2,083,540 za metriki, za mahindi na mchele (mazao yaliyolimwa humu humu nchini pamoja na yaliyonunuliwa toka nje) kwa ziada ya kuuza, mazao yaliyokuwa thamani ya shilingi 1,546,033,253/80 katika kipindi hicho cha miaka kinachozungumziwa. Thamani ya mazao imeonyeshwa katika "Appendix B".

(2) Kuhusu shughuli za mauzo za Halmashauri, fanikio kubwa pia lilipatikana. Halmashauri iliuza mazao yenye thamani ya shilingi 1,720,594,366/- katika kipindi hicho, na mauzo hayo yameonyeshwa katika Appendix "C'.

(3) Orodha ya mauzo yanayoonyeshwa katika "Appendix 'C" inahusikana na ziada ya mazao ya kuuza ambayo yaliuzwa hapa nchini ama nchi za nje. Katika miaka 9 hivi iliyopita, wafanya kazi wa Halmashauri hii wamejifunza jambo moja la uuzaji wa mazao nchi za nje ambalo ni kiini, nacho ni kule kuamua kiasi

cha ziada ya mazao kinachoweza kuuzwa nje, wakati gani, na katika masoko gani. Zoezi hili halikuwa rahisi. Kwanza si rahisi kukisia kwa usahihi kiasi cha ziada ya mazao kinachoweza kuuzwa kwa sababu hazikuwepo hesabu sahihi kwa ukosefu wa Mabwana shamba wa kutosha na wanaoweza kukusanya hesabu za namna hiyo. Hesabu hizo hukosewa kwa kiasi cha 20% mbali na namba iliyo sahihi, hali ambapo katika nchi nyingine kosa hilo hufikia 12 kwa mia tu, na kiwango cha dunia ni 10 kwa mia. Ni rahisi kutoa makadirio ya mazao yaliyo juu ya ardhi, lakini kwa mazao ya chini kama mihogo, karanga, ni vigumu. Pili, lilikuwepo na bado lipo tatizo la biashara iliyo kinyume cha sheria, ifanywayo na wapinga ujamaa wenye zile kasumba za kinyonyaji ambazo huwaendesha wachuuzi. Kuhusu jambo hili, Halmashauri ililazimika kwanza kuwapiga vita makabaila na mabepari wa humu nchini na kuikandamiza biashara yote iliyo ya sheria, halafu ndiyo iweze kuyakabili matatizo mengineyo. Tatu, lilikuwepo tatizo la kubadilika kwa wingi wa mazao kwa ajili ya ugeugeu wa hali ya hewa na mvua. Kama inavyoonekana katika hesabu za mauzo, yamekuwepo mabadiliko ya kusumbua sana katika kiasi cha mazao ya kuuzwa, jambo ambalo limeifanya Halmashauri kuona ugumu kuyatosheleza masoko yetu yaliyopo mapema na kwa wingi wa kutosha. Zaidi ya hayo, tumeyakabili matatizo kuhusu kushindwa kwa wakulima kuchuma na kukusanya mazao yao upesi vya kutosha hasa wakati tunaposhughulika na mazao ya aina ya mbegu za mafuta kwa mauzo ya awali. Ili tuweze kufanya uamuzi kuhusu kupatikana kwa mazao ya kutosheleza mikataba tuliyo nayo chini ya mikataba ya biashara huwa tunategemea sana makadirio tunayopewa na Kilimo, Vyama vya ushirika na matawi ya Halmashauri yetu. Kwa hiyo kufanikiwa au kutofanikiwa katika kukadiria kiasi kitakachopatikana kwa ununuzi kutokana na usahihi wa utabiri wa mazao ufanywao na hao waliokwisha tajwa. Si lazima kuitilia mkazo zaidi umuhimu wa makadirio sahihi ya mazao, kwa maana ukosefu wa makadirio ya kufaa ya mazao ya kuuza utasababisha kutokuweza kupeleka mazao hayo katika tarehe tulizopatana na wanunuzi, na tukio kama hilo litawafanya wanunuzi wetu wa nje kutafuta wauzaji wengine wa kuaminika zaidi, wauzaji ambao ni wale washindani wetu. Kila mara tumesisitiza juu ya umuhimu wa kuyadumisha masoko tuliyo nayo, na mara tupatapo soko lolote

geni, tumekuwa tukijitahidi kulishikilia na kulidumisha moja kwa moja. Ni vibaya kuchukulia masoko ya nje kama mahali pa kutolea ziada au mafuriko ya muda ya mazao yetu, kwa sababu fikara za namna hizi haziwafurahishi kamwe wanunuzi wetu, na zaidi tutakuwa tunaiharibu sifa ambayo Tanzania imekwisha jipatia. Twapenda kutaja hapa kwamba katika miaka michache iliyopita tulipitia hali ambapo maagizo kutoka kwa wanunuzi wa nje yalikuwa makubwa kiasi ambacho hatukuweza kuyatosheleza pamoja na kushibisha mahitaji ya ndani ya nchi kwa kutumia mazao tuliyowcza kuyapata. Hali kama hii inatokea hasa kuhusiana na mazao ya aina ya mbegu za mafuta kama vile karanga. Kwa hivyo sasa tunayaelewa matatizo, na wajibu wetu wa mwanzo ni kuyatatua matatizo hayo. Halmashauri pia imefanikiwa kujipenyeza katika masoko mapya, licha tu kuongeza kiasi cha mauzo katika masoko ya Ulaya ya Magharibi na ya Mashariki, Ujapani, Singapore, Cyprus, Ugiriki, Marikani, Zaire, Burundi, Kenya, Uganda na Zambia. Imekuwa si jambo rahisi kupenya katika masoko haya; ilituchukua kiasi cha miaka kama mitatu au mitano hivi kujijenga thabiti katika masoko menginc kati ya hayo yaliyotajwa. Zaidi ya hayo, Halmashauri hujielimisha kila wakati juu ya masoko ya zamani na mapya ili iwe na habari za kisasa na mpya kuhusu mambo mapya yanayotokana na mabadiliko ya hali katika masoko hayo. Ili kufanya hivyo Halmashauri imekuwa ikijinufaisha na taarifa za kibiashara za masoko hayo, kwani ingalikuwa si jambo la busara kuyatarisha mipango na kuweka lengo kuhusu uuzaji wa mazao nchi za nje kutokana na taarifa zisizokuwa kamilifu au zilizo za wakati uliopita.

(4) Kwa upande wa habari za kuhusu ufanyaji biashara wa Halmashauri, katika miaka hiyo iliyopita Halmashauri inaweza kudai kwamba ilifanikiwa sana, kama inavyoonekana kwenye vitabu vyake vya matumizi na mapato ya fedha, na inavyoonekana katika shughuli nyingine za maendeleo zilizofanywa na Halmashauri. Ili kuongeza juu ya ufanisi wa Halmashauri tutatoa hapa hesabu kuhusu mazao, mali taslimu, na mengineyo, na kiasi cha faida kufuatana na jumla ya mauzo na kima cha fedha zilizoingizwa katika uzalishaji wa faida (investment).

Halmashauri iliilipa Serikali kodi ya kiasi cha Sh. 42,448,760/50 katika miaka ya fedha 1964 hadi 1970. Jumla hii sehemu zake zilikuwa ni kodi ya mazao yaliyouzwa kwa nchi za nje, mchango wa maendeleo na mchango wa Azimio, na kodi juu ya vipato vingine vingine kama faida itokanayo hasa na kodi za nyumba. Zaidi ya kulipa kodi, Halmashauri ilishiriki vema katika mpango wa uzalishaji rasilmali katika nchi, kwa kuingiza kiasi cha shilingi milioni 24½ katika muda wa miaka 1963 hadi 1970; Kuhusu mipango ya kuongeza rasilmali wakati ujao, Halmashauri imekwisha kamilisha mipango yake ya kuweka shilingi milioni 5.4 kwenye uzalishaji wa raslimali (Capital formation) katika miaka 1972 hadi 1974 ya fedha. Zaidi ya uwekaji huo wa fedha kwenye mipango ya uzalishaji wa rasilmali, Halmashauri pia hushiriki kwenye uwekaji fedha kwa kununua hundi za hazina (treasury bills) ambazo hukomaa na kuzaa faida katika muda wa siku 60 hadi 90.

Katika wajibu wake kama chombo cha kuchumia fedha za kigeni, Halmashauri iliichumia nchi kiasi cha shilingi 963,209,229 kutoka mwaka 1964 hadi 1970. Tukichunguza miaka hii ya mwishoni mwa kipindi tunachozungumzia, ambayo inawakilisha vema zaidi wastani wa jumla ya biashara iliyofanywa na Halmashauri katika miaka yote hiyo, tutaona mambo ya kweli ambayo yanathibitisha madai yetu kwamba shughuli na mafanikio ya Halmashauri katika biashara kwa ujumla zilikuwa za kutosheleza. Kwa mfano, mnamo mwaka wa fedha 1967/68, Halmashauri ilikuwa imeshaongeza mali yake taslimu kutoka kima cha chini cha shilingi 1,221,880/- katika mwaka 1963/64 mpaka kiasi cha shilingi 85,995,088. Kiasi hiki kinaonyesha nyongeza kamili ya sehemu 11 ya mia ya kiasi cha shilingi 8,365,425 kilichokuwepo mwaka 1966/67. Katika mwaka 1968/69, mali taslimu kwa jumla zilikuwa kiasi cha shilingi 93,334,545, kiasi ambacho kinaonyesha nyongeza kamili ya shilingi 7,339,357 ama 8 kwa mia juu ya thamani iliyokuwepo katika mwaka 1967/68. Katika mwaka 1968/69 pia ziada kamili iliyotokana na biashara za Halmashauri ilikuwa shilingi 45,313,708/37 kiasi ambacho kilionyesha 14% ya mauzo taslimu, au 48% ya jumla ya mali taslimu zilizokuwepo.

Katika muda wa miaka ya fedha 1965/66 hadi 1969/70, kadiri ya uingizaji na utokaji wa mali ilikuwa 10.2.

Ishara nyingine inayoonyesha fanikio la shughuli zetu za biashara ni ule uingiaji na utokaji wa rasilmali (assets turnover). Katika mwaka 1967/68 kadiri ya kuingia kwa raslimali ilikuwa 2.8, katika mwaka 1968/69 ilikuwa 3.5. Tarakimu hizi za makadirio zinathibitisha kadiri ya mafanikio ya Halmashauri katika kuongeza kima cha mauzo kwa kutumia rasilmali iliyokuwepo wakati huo. Baada ya kulipa kodi na kulipa faida, ziada ama faida taslimu iliyotokana na biashara Halmashauri ilikuwa na shilingi 16,719,968/78 katika mwaka 1968/69 ambayo ni 5.4% ya jumla ya mauzo taslimu yaliyofanyika au 18% ya rasilmali yote iliyokuwepo. Pamoja na mabadiliko yaliyohusika, fanikio la Halmashauri katika miaka 1969/70 na 1970/71 lilikuwa kiasi hicho hicho tukizipima kwa uwiano huo huo.

Kipeo cha mafanikio kilichoelezwa hapo juu kilipatikana kutokana na ushirikiano na bidii ya wakulima pamoja na wafanya kazi wa Halmashauri katika juhudi zao shupavu walizozionyesha kwenye kazi zao mbali mbali kufuatana na moyo na mafundisho yaliyomo katika KANUNI za TANU. Wakati wa kutunga hila na njia zake za kuuza mazao, Halmashauri imekuwa ikijitahidi kuutafuta ukweli wenyewe na hali, kwa kuitegemea kamati ya maongozi (Management Committee) na kushauriana nayo badala ya kutegemea mtaalamu mmoja ambaye anaweza kuwa na chuki za binafsi ama matatizo yake mengine yanayoweza kupotosha ukweli wa mambo. Yafaa pia kutajwa hapa kwamba utegemeaji wa mitindo ya kutumia kamati katika kufanya kazi nao una mipaka yake. Utegemeaji wa kamati hupotoshwa na watu fulani fulani kwa kuzitawala kamati hizo kwa kuzuia utabiri wa ukweli wa hali. Tumekuwa tunatumia njia inayoitwa "Delphi Technique" ambayo hufanyika kwa namna ambayo makubaliano yaliyofikiwa na wataalamu ama viongozi wa idara na sehemu mbali mbali hayaruhusu chuki za kibinafsi kutawala matendo ya kamati. Katika njia hii habari za utabiri hupatikana kutoka kwa viongozi wa matawi (Branch Managers), Wakili wa Biashara (Agents), Wizara mbalimbali, na nchi za nje, na hupitishwa kwa wakuu wa Idara mbali mbali ambazo huzichambua na kuzichuja. Twa-

weza kuwaeleza wasomaji kwamba ingawa utabiri, mkadirio na hesabu si bora kushinda kipaji, wale wanaoitumia njia hii ya "Delphi" wanaweza kutoa matokeo ya kuweza kutegemea.

## SURA YA NNE

## *ULIMBIKAJI WA RASLIMALI*

(1) *Mabohari*: Kwa muda usiofikia miaka kumi tangu kuundwa, Halmashauri ya Taifa ya Mazao imeongeza vifaa vya kuhifadhia mazao, yaani mabohari, kuliko kiasi kilichofanywa wakati wote wa utawala wa Kikoloni. Katika siku hizo za biashara isiyokuwa na vizuizi (free trade) mfanya biashara binafsi hakulazimika kujenga vifaa vya bohari zaidi ya vile alivyohitaji yeye binafsi katika biashara yake.

Halmashauri ya Taifa ya Mazao ilipoanza kazi yake ilikabiliwa na shida za kupata mabohari ya kufaa na ya kutosha. Hata hivyo kuanzia mwaka 1963 Halmashauri imejijengea mabohari ya kuhifadhia mazao yaliyofungwa katika magunia. Kusema kweli, Halmashauri inayo kanuni maalum isiyobadilika ya kuhusu uhifadhi wa mazao, ambayo imeiwezesha kujenga mabohari makuu yaliyopo sasa katika sehemu mbali mbali za nchi.

Ujenzi wa nyumba na vifaa vya maghala pamoja na uundaji mwingine wa raslimali hufanyika kwa kutumia akiba ya rasilmali ya Halmashauri ya mazao ambayo hupatikana kwa kukata kiasi cha 2½% katika bei za mauzo za mazao yote yaliyo chini ya Halmashauri. Kutokana na akiba hii, Halmashauri imeweza kujenga maghala yafuatayo katika sehemu zifuatazo:—

| *No.* | *Mahali* | *Ukubwa* (*Metric tani*) | *Gharama ya ujenzi* (*Shilingi*) |
|---|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam | 35,000 | Shs. 2,349,071/- |
| 2. | Mtwara | 35,000 | Shs. 3,841,519/- |
| 3. | Iringa & Mikumi | 16,300 | Shs. 1,594,024/- |
| 4. | Dodoma | 24,000 | Shs. 2,994,337/- |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5. | Arusha | 18,000 | Shs. 1,175,252/- |
| 6. | Moshi | 14,000 | Shs. 1,635,958/- |
| 7. | Mwanza | 4,500 | Shs. 509,664/- |
| 8. | Mpanda | 9,000 | Shs. 681,062/- |
| 9. | Musoma | 5,500 | Shs. 787,352/- |
| 10. | Manyoni | 4,500 | Shs. 556,572/- |
| 11. | Tanga | 5,000 | Shs. 723,388/- |
| 12. | Singida | 4,500 | Shs. 556,528/- |

Uwezo wa Halmashauri wa kuweka mazao kiasi cha tani 175,300 umetokana na fedha ambazo Halmashauri yenyewe imezipata kutokana na akiba yake ya ndani bila kutegemea misaada yoyote ya fedha kutoka nje. Hii inaambatana na siasa yetu ya kujitegemea.

(2) *Mipango inayoendelea*:

Kwa hivi sasa, Halmashauri ingali inajenga ghala mbili zaidi, moja mjini Dar es Salaam na nyingine huko Mtwara zote kwa jumla zikiwa na uwezo wa kushika karibu tani (metriki) 32,000.

(3) *Mahitaji ya Maghaa kwa wakati ujao*:—

Kufuatana na uongezekaji wa kila mwaka wa Mazao mbali mbali na uongezekaji wa kiasi cha ziada ya kuuza cha Mazao ya kila aina, Halmashauri imenuia kujenga ghala nyingine zaidi. Bila shaka ni lazima tutambue kwamba uongezekaji wa rasilmali yetu ni pole pole kuliko kuzidi kwa mahitaji ya Maghala kwa jinsi miaka inavyoendelea, hasa kuhusu mazao kama maharagwe, mihogo, mtama, uwele na mengineyo ambayo yameingizwa katika orodha ya Mazao yaliyo chini ya Halmashauri ya Taifa ya Mazao.

Hata hivyo, ifuatayo ni orodha ya ghala zitakazoongezwa:—

| *Mahali* | | *Ukubwa wa ghala (tani)* |
|---|---|---|
| Arusha | | 20,000 |
| Dodoma | | 10,000 |
| Morogoro | | 20,000 |
| Tabora | | 20,000 |
| Kigoma | | 10,000 |
| | Jumla | 80,000 |

Kutokana na ghala zilizopo, kwa wastani Halmashari huokoa shilingi 25/- kwa kila tani kwa msimu ambazo ingelipa ingalikuwa inatumia ghala za kukodi. Hata hivyo ukubwa wa ghala zilizopo pamoja na zile zitakazoongezwa hushika 50% ya jumla ya mazao yote yanayopitia kwenye Halmashauri kila mwaka.

(4) *Mpago wa ghala za mahandaki (silos project)*

Hii ni njia mpya ya kuhifadhi mazao kwa wingi, badala ya njia ya kawaida ya uwekaji wa kutumia magunia au mifuko. Ukubwa wa ghala hizo ulikisiwa kuwa tani 40,000 mpaka 60,000 ambazo kwa jumla zitagharimu shilingi 45,000,000/-.

(5) *Uongezaji mwingine wa raslimali:—*

Rasilmali nyingine zinazohusu maghala ya kuhifadhi mazao, matunzo bora ya mazao hayo na kushughulikia mazao kwa ujumla zimeingizwa katika mipango ifuatayo:—

(i) Turubai za kufunika mazao yangalipo katika ghala za wazi ama katika kusafishwa. Aina na vipimo mbalimbali vya turubai zimewahi kununuliwa, kwa gharama ya shilingi 1,000,000/-.

*(iii) Ufukizaji na dawa za wadudu:—*

Kuhusu jambo hili gharama zimeingia katika kununua vifaa kama bomba za kufukizia dawa na kadhalika.

(iv) Vifaa vinginevyo:— Vifaa kama mitambo ya kuinulia magunia au masanduku ya mazao, mashine za kupimia daraja za mazao mbali mbali (grading machines), mitalimbo, vigari vya mizigo, mashine za kupima na za kukausha unyevunyevu wa mazao, chekecheke, bomba za kuzima moto, au mizani za kupimia uzito, vyote vimeigharimu Halmashauri, shilingi 3,000,000/-.

Kwa hiyo vifaa ambavyo husaidia katika kazi ya kuhifadhi mazao ghalani kwa jumla vimegharimu Halmashauri kiasi cha shilingi milioni nne au tano hivi.

(6) *Kushiriki katika mipango ya Maendeleo:—*

Halmashauri inakata senti 5 kwa kila kilo ya korosho iliyouzwa mwaka 1970/71 na 1971/72 kama mchango wa maendeleo utakaotumika kutengeneza barabara ndogondogo na mipango mingine katika mikoa inayolima zao la Korosho. Jumla ya fedha hizo ni shilingi 4.8 milioni katika mikoa ya Pwani, Mtwara na Ruvuma.

(7) *Uongezaji wa mali Taslimu:—*

Halmashauri imeendelea sana katika kupanua rasilmali yake taslimu. Mwaka ilipoanzishwa, 1964/65 mali taslimu kuhesabu majumba, viwanja, mashine na vinu, magari na vifaa vya ndani ya majumba na zana nyingine zilifikia kiasi cha shilingi milioni 1.8 tu, lakni mwaka wa 71 mwezi wa tano tarehe 31, hesabu hii ilikuwa imeshafikia 22.8 milioni, yaani iliongezeka kwa shilingi milioni 21. Kadiri ya shilingi milioni 3.8 zimekuwa zinatumika kila mwaka kuongeza mali taslimu za Halmashauri, yaani mwongezeko wa 20 kwa mia kwa kila mwaka.

## *SURA YA TANO*

## *HALMASHAURI BAADA YA AZIMIO LA ARUSHA*

(1) *Vinu vilivyotaifishwa:—*

Katika mwaka 1967 yaani mwanzo wa hatua za kutaifisha mali zilizofuata kutangazwa kwa Azimio la Arusha, Vinu vingi vilikabidhiwa Halmashauri ya Taifa ya Mazao na muswada wa sheria ya kutwaa mali na kuipa Halmashuari ya Taifa ya Mazao, muswada wa mwaka 1967. Matokeo ya sheria hii ni kuwa iliiongezea Halmashauri wajibu wa kuhakikisha na kuendeleza uongezekaji na uuzaji wa mazao makuu ya Tanzania na kuyatengeneza tayari kwa kununuliwa na watu. Katika kutekeleza kazi hizi Halmashauri ililazimika kuyapatanisha au kuyalinganisha masilahi ya wakulima pamoja na yale ya walaji.

Hata mtu hana haja kusisitiza kwamba siasa ya ujamaa, ilikuwa ndiyo kiini cha Azimio la Arusha, ilitilia mkazo maalum juu ya kilimo. Wakati wa kuikabidhi Halmashauri rasilmali na madeni ya vinu vilivyotaifishwa serikali iliweka maanani haja ya kupanga uzalishaji na utengenezaji mazao, usafirishaji, na ugawaji wa mazao ya vyakula, ili kuwafanya wakulima na walaji wawe na uhusiano zaidi. Mnamo mwaka 1968, wakati shirika la Taifa la Vinu vya usagaji wa mazao (National Milling Corporation) lilipoanzishwa, rasilmali na madeni yote ambayo ile sheria ya kutoa mali ya 1967 ilikuwa imeyakabidhi Halmashauri sasa yalikabidhiwa shirika hilo jipya. Na hii ndiyo habari iliyohusu vinu vilivyochukuliwa na serikali.

(2) *Kuuza mazao nchi za nje kwa misingi ya siasa ya ujamaa.*

Katika nyakati za kabla ya Azimio la Arusha, Halmashauri ilikuwa na desturi ya kuuza mazao yake nchi za nje kupitia kwa watu hao ilifikiriwa kuwa haukuambatana na ujenzi wa siasa ya ujamaa. Halmashauri ilifuatisha siasa ya serikali kwa kufanya mauzo kwa njia zinazofuatana na ujamaa. Njia hizo mpya ziliambatana na kufutilia mbali wale wanadi pamoja na wakili wa

matajiri, na kufunguliwa kwa idadi maalumu katika Halmashauri, ya kuuza ng'ambo moja kwa moja bila ya kupitisha kwa watu fulani fulani. Kwa njia hii utafutaji wa nafasi ya mazao katika Halmashauri hadi bandarini, kugharamia shughuli za uuzaji wa mazao hayo na matayarisho mengine yote ya mipango ya mauzo sasa ilifanywa na Halmashauri. Siasa hii ya kugeuza uuzaji wa mazao kufuata njia za kijamaa msingi wake ulikuwa ni ile haja ya kuwaondosha wachuuzi wote wa kati waliokuwepo kati ya Halmashauri na wanunuzi, na haja ya kuchuma fedha za kigeni kwa wingi, kulinganisha na zamani ambapo kiasi cha fedha hizo kilitegemea ambacho wale wapiga mnada na wakili wa biashara wa matajiri wa ng'ambo waliwatoza wanunuzi. Kuhusika kwetu katika uuzaji wa moja kwa moja wa mazao yaliyo chini yetu kumetuwezesha na kutunufaisha zaidi kuwafunza wafanya kazi wetu juu ya matatizo ya biashara katika kuuza mazao yetu nje.

(3) *Ushirikishwaji wa Wafanyakazi.*

Katika kuwashirikisha wafanya kazi katika uongozi wa kazi kufuatana na toleo No. 1 la Rais la mwaka 1970, Halmashauri imefungua mabaraza ya wafanya kazi katika makao yake makuu na matawi yake yote. Mikutano ya mabaraza hayo ya wafanya kazi imejadili na kupambanua mambo muhimu sana yahusuyo utendaji wa kazi za Halmashauri, na kupasisha njia za vitendo za kutatua matatizo fulani fulani ya Halmashauri. Wajumbe wa wafanya kazi katika mabaraza hayo wanazidi kufahamu ya kuwa wanao wajibu mkubwa katika kuunda katiba za kazi na kwamba wafanya kazi waliowachagua wanautegemea uongozi wao na kutumaini kwamba watakuwa watu wa kuujali wajibu. Imehisiwa pia kwamba upeanaji wa habari lazima uwe wa njia mbili toka kwa viongozi na kwa wafanya kazi, kama mabaraza ya wafanya kazi yanatimiza kazi zake barabara. Licha tu ya kubadilishana mawazo, mabaraza hayo ya wafanya kazi yamewafanya wale wanachama wake kutambua kwamba cheo huambatana na madaraka na kwamba ili kuongoza kazi vema lazima mtu aelewe sio tu jinsi Shirika linavyofanya kazi zake, ila pia aelewe maana ya uamuzi au mashauri mbalimbali yafanywayo na shirika hilo katika uendelezaji wa shirika. Kwa ujumla, kazi ya kuwashirikisha

wafanya kazi katika kufanya mashauri ya Halmashauri hii imeonyesha kuwa wafanya kazi wanaendelea kutambua kwamba Mashrika ya Taifa yanamilikiwa na wote, na kwamba ni kwa ajili ya maslahi yetu wote kuhakikisha kwamba maongozi yake ni thabiti.

(4) *Mwongozo wa TANU*:

Kutangazwa kwa Mwongozo mpya wa TANU na kuanzishwa kwa Jeshi la Mgambo kumepokelewa vema sana katika Halmashauri hii. Zaidi ya wafanya kazi 185 wa Halmashauri wamekuwa wakipewa mafunzo ya kijeshi na waliobaki watapewa mafunzo hayo kwa zamu mpaka wafanyakazi wote wawe wamepitia mafunzo hayo. Hii inaonyesha kwamba mwitiko wa Halmashauri kwa kifungu cha 26 cha Mwongozo wa TANU umekuwa mfano bora, na inaonyesha dhamira ya wafanya kazi wetu kuhusu umuhimu wa ulinzi na usalama wa Taifa.

(5) *Elimu kwa Wafanyakazi Kazi.*

Halmashauri inajitayarisha kuanzisha mpango mathubuti wa kuwaelemisha wafanya kazi wake. Hatua ya kwanza itakuwa ya kuondoa ujinga wa kutojua kusoma na kuandika baina ya wafanya kazi wetu, wengi wao wakiwa chini ya mpango huo. Zaidi ya hayo, Toleo namba 1 la Rais litaelezwa na maana yake itajadiliwa. Ili kuwajulisha viongozi wote wa Halmashauri juu ya kazi na shughuli za Halmashauri kwa kinaganaga, mafunzo maalum yatatolewa kuhusu kazi za Halmashauri, sababu za kuanzishwa kwa Halmashauri, mwuundo na wajibu wake katika kujenga na kuibadilisha jamii. Kwa njia hii tunatumaini kuwatayarisha viongozi wetu kwa shida za siku zijazo na kwa kulijenga taifa kwa matendo kutokana na kuelewa na kujua madhumuni ama wajibu wa Halmashauri yetu. Ni imani yetu kwamba kila jitihada itafanywa ili kuvitumia vipawa ama uwezo wa binadamu katika nchi hii kwa kuendeleza elimu na ujuzi au ufundi unaotakiwa kwa ajili ya maendeleo ya wafanyakazi wote ili kulifikia lengo letu la maendeleo na kuongeza uzalishaji wa mali.

(6) *Ushirika wa Ujamaa*:

Mojawapo ya shabaha kuu za Halmashauri hii ni kuvipa nguvu vyama vya Ushirika. Hii hufanyika kwa kuvifanya vyama vikuu vya Ushirika kuwa ndio wakili wa Halmashauri nchini, na vyama vikuu hivyo kuvitumia vyama vidogo vya Ushirika kuviwakilisha. Hivi, Halmashauri huunga mkono uwamuzi wa wizara ya Kilimo na Ushirika kwamba vijiji vya ujamaa yafaa vijiunge kuwa vyama vidogo vya Ushirika. Halmashauri itavihifadhi vyama hvyo vya Ushirika na vijiji vya Ujamaa kwa misaada yote inayowezekana ambayo itatumika kuwezesha vyama hivyo kuuza mazao ya Kilimo yanayolimwa katika vijiji hivyo. Halmashauri hutambua barabara kuwa kuimarisha soko la ndani kwa upangaji mauzo kunakofanyika na vyama vya Ushirika kunaweza kuwa na uzito mkubwa sana katika maendeleo ya nchi.

(7) *Muungano wa Mashirika yauzayo Mazao*:—

Majadiliano kuhusu urekebishaji wa shughuli za uuzaji wa Mazao za Halmashauri mbali mbali, yamekuwa yakiendelea tangu kuteuliwa kwa Tume ya Rais ya Uchunguzi iliyochunguza mwenendo wa Vyama vya Ushirika na Halmashauri zinazouza Mazao mnamo mwaka 1965. Majadiliano hayo yamemalizika katika tamko la hivi karibuni la Wilazara ya Kilimo na Ushirika kwamba kazi za utayarishaji wa mpango ya kuanzisha mashirika makubwa mawili ya mauzo zimekwisha fanyika. Uamuzi huu unashangiliwa sana hasa tufikiriapo kuwa unamaanisha kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za uongozi wa mashirika, na kwamba shabaha yake ni kupanua soko la ndani la nchi na kuongeza na kufaidika soko la wanunuzi wa ng'ambo. Hii pia inthibitisha kuwa serikali inajua wazi kwamba katika orodha ya fedha za maendeleo, kuongezeka kwa fedha za kigeni ni kwa lazima ili mipango yetu ya maendeleo itimizike, na kwamba Kilimo ndiyo asili ya fedha hizo. Uharakishaji wa mapinduzi ya Kilimo katika nchi hii kwa kuongeza mazao hauna budi uambatane na masoko bora yaliyopangwa vizuri na thabiti pamoja na kupanuliwa kwa soko la ndani ya nchi. Ushirikishaji wa wakulima wa kiasili (Subsistence farmers) katika kuendeleza ukulima wa kisasa na wa njia za kisasa za kutoa mazao na kuyauza, ni hatua muhimu sana ya kuelekea katika maendeleo.

## *SURA YA SITA*

## *MAENDELEO YA VIONGOZI NA UTAYARISHAJI WA VIONGOZI WANANCHI*

Katika siku zake za mwanzo, Halmashauri ilikabiliwa na tatizo la kuwapata viongozi wananchi wenye ujuzi wa kutosha kushika nafasi za kati na za juu za uongozi wa Halmashauri. Haja ya kupata viongozi wananchi wenye ujuzi iliongezeka zaidi wakati madaraka ya Halmashauri yalipopanuliwa zaidi na orodha ya mazao yaliyo chini ya Halmashauri kuongezwa. Pale awali Halmashauri iliikuwa ikiongozwa na watu ambao si wananchi, wengine walijifunzia katika Mashirika ya biashara za binafsi. Hata hivyo ilitambulika kwamba siasa ya serikali ilikuwa kuwafunza Watanzania wananchi humu humu nchini ama ng'ambo ili waweze kuchukua madaraka ya uongozi katika Halmashauri kutoka kwa wale viongozi wageni. Ili kufikia lengo hili, wafanya kazi wapya walipokelewa kutoka mashuleni na vyuoni na kupewa mafunzo upya hapa nchini na ng'ambo na pia kupewa mafunzo wangali kazini, ya uongozi wa Shirika kubwa la biashara.

Hivi leo uingizaji wa wananchi katika kazi za maongozi ya Halmashauri umetimizika. Idara zote nane za Halmashauri zinaongozwa na wananchi: Halmashauri haina mikataba yoyote ya maongozi "Management agreements" na shirika lolote la nje, wala haliamini kuwa ni lazima kuajiri wataalamu washauri (Consultants). Ukweli uliopo kwamba Halmashauri imekuwa inaongozwa na wananchi unaonyesha kuwa ukipewa muda na tukinuia tunaweza kuzifikia shabaha zetu za kisiasa na za uchumi.

Uongozi wa Halmashauri sasa una watu 1,300, na kadiri mazao yanavyoongezeka, hesabu hii haina budi kuongezeka. Halmashauri inao wajibu wa kutayarisha mipango kamili ya kufunza viongozi ili kuwatayarisha viongozi hao kutoa utumishi bora zaidi kwa Halmashauri na taifa kwa jumla.

Kimechapwa na : Nuta Press Ltd. P.O. Box 323, Dar es Salaam